JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
(TAMISEMI)
MTIHANI WA KABLA YA UTIMILIFU KIDATO CHA SITA
(IFAKARA SEKONDARI)
KISWAHILI 2
(Kwa watahiniwa walioko na wasiokuwa shuleni)

Muda: Saa 3 SEPTEMBER 2024

---

Maelekezo kwa Watahiniwa

1. Mtihani huu una sehemu A na B zenye jumla ya maswali nane (8).
2. Jibu maswali yote sehemu A na sehemu B jibu maswali matatu (3) swali la tano (5) ni la lazima.
3. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.

Mtihani huu una kurasa tatu zenye maandishi

SEHEMU A (ALAMA 40)

Jibu maswali yote kutoka sehemu hii.

1. Fafanua kauli isemayo “Ujamala wa fasihi simulizi hauwezi kuwa na ujamala wa fasihi andishi” ukitegemea kwenye nduni bainifu za fasihi simulizi kwa kutumia hoja tano (5)
2. Riwaya pendwa na riwaya dhati hutofautiana katika faida kwa jamii husika. Onesha sifa tano (5) za riwaya pendwa ambazo hazipo kwenye riwaya dhati.
3. Eleza maana ya dhana zifuatazo
   (i) Mhusika kivuli
   (ii) Mahadhi
   (iii) Kongozi
   (iv) Taniaba
   (v) Taswira
4. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha fafanua mbinu za kifani zilizotumika.

Watu wote walikua wakishangilia kwa kofi, miunzi, vigelegele na hoi hoi. Mradi ghasia za kike kwa kiume. Taa za pale penye zulia katikati ya ukumbi ziliwashwa, miale ya mwangaza ilimiminika kutoka juu na kuanguka hapo. Sasa Maimuna alikuwa kaketi nyuma ya jukwaa. Alikuwa kavaa gauni refu lililokokota mpaka chini lenye rangi ya feruzi inayometameta kwenye taa. Kafunga shore la kuvutia.

Muziki ulianza kugongwa kwa mahadhi ya rumba. Maiumuna katikati ya shangwe aliteremka vidaraja kuelekea pale kwenye zulia katikati ya ukumbi. Njia alipokea kikuza sauti kutoka kwa yule mtangazaji, akaanza kuyumbayumba kwa madaha. Alibembea na mdundo huku mwili wake kaulegeza na macho yanasinzia. Muziki ulipofika mahala fulani alianza kuimba.

Nina kovu, ninakovu, wanitonesha kwa inda

Ukikatazwa maovu, warudi waenda yatenda? wanitia

roho mbovu, kwa sababu nakupenda?

Nakupenda nakupenda, kwa sababu nakupenda.

Hapo aliitikiwa na wenzake. Tena mziki ukampokea kwa matao yale yale, na tena wakati ulipowadia aliingia katikati mizani yake

Kama hunitaki tena, usiende nami kwa hila, La
Kwanza si maungwana, na la pili sio mila, Jambo

La kudanganyana, ni jambo lenye madhila, La Madhila

madhila, jambo lenye madhila

Aliitikiwa na kikosi chake. Tena ukafuata muziki, kisha aliendelea huku ukumbi ukipiga kofi kushangilia

Utakaa na wenzio, na kukaa kwa kucheka,
Kumbe moyo wako sio, umekwisha
Kuzunguka, kama zina ufunguo, nyoyo

Zingefedheheka, fedheheka, fedheheka, nyoyo

zingefedheheka.

Shangwe la ukumbi lilifuata, kama kawaida, baada ya kuitikiwa na kikosi ulifuata muziki kama mwanzo. Maimuna aliendelea

Shone sanda, sanda, na kiuzo cha ubao,
Uwaalike vijana na watu uwatakao,
Unizike ni kijana, ukae na uwapendao,
Wapendao wapendao, ukae na

Uwapendao.

Hapo muziki ulibadilika gafla. Naamu Maimuna mdeniko kweli. Alidemka yeye mzima. Yakacheza mabega. Ikapunga mikono, ikakatika shingo kichwa...... vyote vilicheza kama ngoma ilivyomuamrisha. Kofi, kelele, mbinja, vicheko, furaha vigelegele. Mdemko ulizidi na watu walizidi kushangilia. Na iwe huo wimbo ambao ndio ulimfuma pabaya. Bwana Maksudi, alikuwa akilowa kifua chake machozi. Hakuweza kuzizuia hisia zake. Alilia taratibu kwanza, halafu sauti ilizidi kuwa kubwa, akilia kwa kwikwi. Rashid aliyetekwa na mikogo ya Maimuna, hakujua vipi, alimwona Maksudi na mkongojo wake na huku akiinua mkono mmoja, alishika njia ilioelekea pale katikati ya ukumbi. Maimuna alipokuwa akicheza. Maksudi alikuwa akienda mwili tu hahisi chochote. Hakujua alilokuwa akifanya. Alijikongoja ajabu kwa kila mtu.

“Tazama, tazama” watu walianza kuoneshana, “Tazama mzee yule anakwenda wapi”? Anawazimu nini! kuna nini! Lakini Maksudi na mkongojo wake taratibu alisogea mbele. Muziki ulisita kwa ghafla.

SEHEMU B (ALAMA 60)

Jibu maswali matatu (3) kutoka sehemu hii swali la tano (5) ni la lazima.

ORODHA YA VITABU

(A) USHAIRI

| | | |
|---|---|---|
| Kimbunga | - | Haji G. Haji |
| Mapenzi Bora | - | Shaban Robert |
| Chungu tamu | - | Theobald Mvungi |
| Fungate ya Uhuru | - | Mohamed S. Khatibu |

(B) RIWAYA

| | | |
|---|---|---|
| Usiku utakapokwisha | - | Mbunda Msokile |
| Kufikirika | - | Shaban Robert |
| Mfadhili | - | Hussein Tuwa |
| Vuta N'kuvute | - | Shafi Adam Shafi |

(C) TAMTHILIYA

| | | |
|---|---|---|
| Kwenye Ukingo wa Thim | - | Ibrahim Hussein |
| Morani | - | Emmanuel Mbogo |
| Kivuli kinaishi | - | Said Mohamed |
| Nguzo Mama | - | Penina Muhando |

5. Fafanua upekee wa mwandishi wa kazi za fasihi jinsi unavyojidhihirisha katika kazi zao. Toa hoja nne (4) kutoka kila Diwani mbili ulizosoma.

6. Waandishi wa Tamthiliya wamejadili malalamiko ya wasionacho dhidi ya maisha yao ya kila siku kwenye kazi zao. Unadhani wasionacho wananalalamikia nini? Toa hoja nne (4) kutoka kila tamthiliya mbili ulizosoma darasani.

7. Waandishi wa kazi za fasihi wana mbinu maridhawa ambazo hulenga kuzitoa kwa jamii zao kutoka kwenye matatizo mbalimbali yanayowakabili na kuzionesha mwanga. Thibitisha usemi huu ukitumia Diwani mbili ulizosoma kwa hoja nne (4) kutoka kwenye kila kitabu

8. "Wasanii hutumia kipengele cha lugha kwa kuwa ndio uti wa mgongo wa kazi zao". Kwa kutoa hoja nne (4) kutoka kwa kila Riwaya mbili (2) ulizosoma fafanua dai hili kupitia kipengele cha Jazanda.